

TRL wakataa
mwekezaji
mwingine ▶ 2



Mwanajeshi aona
kwa kutumia
ulimi ▶ 3



Mahakimu
wazidi kuikimbia
kesi ya Deci ▶ 8

Wasomaji wetu
wapendwa

Gazeti lako ulipendalo la
Mwananchi kuanzia Machi
22, 2010 litauzwa Sh500 tu.
Tunawashukuru sana kwa
kutuunga mkono na ku-
waahidi kuwa tutaendelea
kuwaletea habari zenye
kelimisha, kuhabari-
sha, kuburudisha na
uhakika.

MWANANCHI

www.mwananchi.co.tz

Bei: TSh. 400 Kenya KSh35

Jumatano Machi 17, 2010

ISSN 0856-7573 Na 03560

Utapiamlo kuua watoto 43,000 mwaka huu

Exuper Kachenje

MASHIRIKA mawili yasiyo ya kiserikali yametangaza kwamba mwaka huu watoto karibu 43,000 watafariki nchini katika umri mdogo kwa utapiamlo.

Taarifa iliyotolewa kwa pamoja na mashirika hayo, Policy Forum na Sikika jana, vifo hivyo vitasababishwa na kukosa chakula bora. "Mwaka 2010 utapiamlo utasababisha vifo vya watoto 43,000," ilisema sehemu ya taarifa hiyo ikimkariri Mkurugenzi wa Sikika, Irenei Kiria.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo Tanzania ina watoto wenye utapiamlo wanaofikia 2.4 milioni na kwamba ni nchi ya tatu miongoni mwa nchi za Afrika zilizoathiriwa zaidi na utapiamlo. Kiria alibainisha kuwa katika muongo mmoja uliopita

watoto zaidi ya 600,000 wenye chini ya umri wa miaka mitano walifariki kwa utapiamlo nchini.

Alisema kiwango cha juu cha utapiamlo kinasababisha kifo, ingawa ni mara chache watoto kufariki kwa njaa akibainisha kuwa wengi wa watoto hao wanafariki kwa sababu lishe na vyakula vyao havina virutubisho vya msingi vinavyohitajika kujenga mfumo imara wa kinga za mwili.

Naye mratibu wa Policy Forum Semkae Kilonzo alisema utapiamlo hudhoofisha pia uchumi wa taifa na kutia hasara ya asilimia 2.6 ya pato la taifa kwa mwaka kutokana na wafanyakazi na wakulima kushindwa kutoa nguvu za kutosha hivyo kupata mavuno machache na kupungua kwa tija ya wafanyakazi.